HISTORIA YA KITENGO CHA ELIMU YA AFYA KWA UMMA

Kitengo cha Elimu ya Afya kwa umma kilianzishwa rasmi na Wizara ya Afya mwaka 1957 Kiongozi wa kwanza wa Kitengo alikuwa Daktari M.S.G. Moller, (Mwenyeji wa Sweden), wakati huo kilifahamika kama Idara ya Elimu ya Afya.

Idara hii ya Elimu ya Afya ilianza kazi yake ikiwa na wafanyakazi waasisi watano, ambao ni:

1. Daktari Mwandamizi – M.S.G. Moller – Mkuu wa Idara
2. Kiongozi bwana Afya – Collin Urqart,
3. Afisa Muuguzi ufuatiliaji- N. Catherine
4. Mchapishaji Mwandamizi – A. Kahangi
5. Mpiga mashine – Philipo Daniel

Pia kulikuwa na:
1. Dereva – Ali Kilindo
2. Tarishi – S. Kipende.

Idara hii ilianzia shughuli zake katika majengo ya hospitali ya Ocean Road ambayo kipindi hicho ilikuwa ikiitwa European Hospital. Ilipofika mwaka 1959, Idara ilihamishia ofisi zake katika maeneo ya hospitali ya Muhimbili, wakati huo ikijulikana kama ‘Princes Margreth Hospital’. Ofisi hizi ndizo zinazotumika kwa shughuli za Kitengo hadi sasa, ambapo baada ya Serikali kuhamishiwa Makao Makuu ya Serikali Mjini Dodoma, bado kuna kiwanda cha uchapishaji, Studio ya Radio na Televisheni pamoja na na kituo cha kupokea simu “Afya Call Centre”.

Kazi kubwa ya Idara ya Elimu ya Afya ilikuwa ni kubuni na kutengeneza vielelezo kwa ajili ya kuelimisha jamii masuala

ya Afya. Idara hii ilikuwa inatoa vipeperushi vilivyochapishwa na *Government Press* kwani Idara haikuwa na mashine ya uchapishaji. Katika kipindi hicho pia kulikuwa na utengenezaji wa *teaching kit*, ambazo zilikuwa zinawekwa vielelezo mbalimbali pamoja na kitabu cha mwalimu ambacho kilitumika kufundishia katika jamii.

Wafanyakazi wa afya walikuwa wakitumia vielelezo hivi kufundishia sehemu mbali mbali, zikiwemo kliniki za mama na mtoto, shule, kampeni dhidi ya milipuko ya magonjwa ya kuambukiza na kwenye shughuli za maonyesho ya kitaifa.
Vielelezo hivyo vilikuwa vikiandaliwa kulingana na hali halisi, mazingira, mila na desturi za wananchi husika. Maradhi ambayo yalikuwa yakisisitizwa na kuelimishwa ni kama vile kuharisha, utapiamlo,ukoma na kifua kikuu. Kazi kubwa nyingine ilikuwa ni kutembelea katika Sehemu mbalimbali mikoa yote mjini na vijijini ili kutoa Elimu ya Afya. Njia nyingine za kuelimisha ilikuwa ni kutumia *Slide Projector* na *Movie film* ambazo zilikuwa hazina rangi (black and white).

Mwaka 1968 Idara ilipata msaada wa automatic mashine kutoka UNICEF ambayo ilisaidia ufanisi wa kazi tofauti na ilivyokuwa ikitumia silk printing mashine, pia WHO waliweza kusaidia Kitengo misaada ya kamera, vifaa vya kuchorea na kadhalika.
Mkutano wa Iringa miaka ya sabini mwanzoni ambao ulihusu kujadili mfumo wa Elimu ya Afya kwa Umma nchini ndio uliopelekea ulioibua mapendekezo kutoaka kwa washiriki ya kuanzishwa kwa Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma na sio Idara tena. Ilipofika mwaka 1978, Idara ya Elimu ya Afya ilibadilishwa jina na kuitwa Kitengo cha Elimu ya Afya kwa Umma kufuatia mapendekezo ya mkutano uliofanyika Iringa.

Mwaka 1985 Kitengo kilianza kupata matatizo ya ufinyu wa bajeti, pesa zilizokuwa zikitolewa zilikuwa hazitoshi. Hii ilichangiwa na kukosekana kwa msaada wa malighafi kwa ajili ya kutumia katika kutengeneza vielelezo, ambao hapo awali ulikuwa ukitolewa na UNICEF. Kwa kipindi hicho mkataba na UNICEF ulikuwa umeisha hivyo misaada ya vifaa mbalimbali haikuwepo tena.

Kwa kipindi hicho majukumu ya Kitengo yalikuwa yafutayo:-

- Kutayarisha miongozo ya Utekelezaji wa shughuli za Elimu ya Afya hapa nchini.
- Kuandaa na kutekeleza mipango ya kuelimisha jamii kwa kutumia njia mbalimbali kama radio, televisheni, kuchapisha vitabu, mabango,vipeperushi na magazeti.
- Kuratibu mafunzo ya wataalam wa fani ya Elimu ya afya ambao walitumika kuelimisha jamii katika ngazi za wilaya na kata.
- Utekelezaji wa miradi ya kuelimisha jamii kama wa uimarishaji na usambazaji wa Elimu ya afya nchini, mradi wa mawasiliano wa Uzazi wa mpango, Uzazi salama, miradi ya kudhibiti magonjwa ya kuharisha na malaria.

Wadau na washirika mbalimbali ambao walikuwa wakishirikiana kwa karibu sana na Kitengo cha Elimu ya afya kwa wakati huo ni UNICEF, WHO, DANIDA, USAID, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Elimu,Wizara ya maendeleo ya jamii wanawake na watoto, Redio Tanzania pia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Taasisi ya Vielelezo na Mashirika ya dini.

Wakuu wa Kitengo waliowahi kushika nafasi ya uongozi katika Kitengo cha Elimu ya Afya ni:

1. Dr. M.S.G. Moller	1957 - 1964
2. Dr. S. J. Mamuya	1964 - 1972
3. Dr. E. Z. Mfinanga	1972 - 1976
4. Mr. I. V. Mbaga	1976- 1983
5. Mr. S. Chizenga	1983 - 1987

6. Dr. G. Mduma	1987 - 1991
7. Dr. H. S. Kasale	1991- 1994
8. Mr. G. Mtavangu	1994 - 1995
9. Dr. G. Mwaipopo	1995 - 1998
10. Dr. G. Kiangi	1998 - 2000
11. Mr. S. Kiluvia	2001 - 2004
12. Dr. G. Kiangi	2004 – 2013
13. Hellen Semu	2013 – 2016
14. Said Makora	2016 – 2018
15. Dr. Amalberga Kasangala	2018-Mpaka sasa

Baadhi ya kampeni mbalimbali ambazo Kitengo cha Elimu ya Afya kiliwahi kuanzisha ni kama ifuatavyo:

1. Kampeni ya Mtu ni Afya
2. Kampeni ya chakula ni uhai
3. Kampeni ya Magonjwa ya zinaa (Gonnorhea)
4. Kampeni ya kipindupindu
5. Kampeni ya chanjo
6. Kampeni ya Uzazi wa mpango (Nyota ya Kijani, Jithamini…n.k.)
7. Kampeni ya UKIMWI (Juliana, Tupo wangapi…….n.k)
8. Kampeni ya Afya ya Uzazi; Jiongeze Tuwavushe Salama, Naweza,
9. Kampeni ya Magonjwa ya Mlipuko (Ebola, COVID 19)

Changamoto kwa kipindi hicho zilikuwa kama ifuatavyo:

1. Upungufu wa pesa kutoka Wizara ya Afya (Serikalini)
2. Kuisha kwa Mkataba wa UNICEF ambao ulikuwa ni msaada mkubwa kwa kupata vifaa na pesa kwa ajili ya shughuli za elimu ya Afya. (mfano mashine zote zilizopo mpaka sasa ni msaada kutoka UNICEF)
3. Uhaba wa wataalam wenye ujuzi pia ilikuwa ni changamoto.

4. Upungufu wa vitendea kazi kama vile vifaa vya kisasa vya mawasiliano, vifaa vya printing (Mashine) na vifaa vya kisasa vya studio.

Mafanikio katika kipindi hicho:-

1. Miongozo.
2. Kitengo kiliweza kuendesha mradi wa water and sanitation, mradi wa Uzazi wa mpango (maarufu kama mradi wa Nyota ya kijani) na mingineyo.

3. Mwaka 1987 Kitengo kilianzilisha maadhimisho ya kitaifa ya siku ya afya duniani, ambayo yanaendelea hadi hivi sasa. Pia Kitengo kimefanikisha Kuanzishwa kwa maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya UKIMWI duniani, siku ya Ukoma duniani, siku ya kifua kikuu duniani na siku ya kutokutumia Tumbaku duniani.

4. Uanzishwaji wa mradi wa ukweli kuhusu maisha, mwaka 1987.

5. Uanzishwaji wa kipindi cha redio kilichoitwa maisha marefu, maisha matamu tangu mwaka 1964 na kubadilishwa jina mwaka 1982 na kujulikana kwa jina la ‘Siri ya Afya bora’, mchezo wa radio wa Zinduka na Kipindi cha Tambueni.

6. Mwaka 1994, kitengo Kilifanikisha/kimewezesha uanzishwaji/Kuanzishwa wa/kwa kozi ya Elimu ya Afya katika chuo cha Elimu ya Afya ya Msingi, Mkoani Iringa.

7. Kuanzishwa kwa Kamati mfano Kamati ya sheria ya Tumbaku na Kamati ya ya Elimu ya Afya ya kuangalia ubora wa vielelezo.

Mpaka sasa 2020, Kitengo kina jumla ya wafanyakazi 28, waajiriwa na wakujitolea…….waliofuzu na wenye uzoefu katika fani ya afya, mawasiliano, utangazaji, uandishi wa habari, sayansi ya jamii, uhasibu, na uchapaji. Kitengo kina sehemu kuu tano ambazo ni:-

- Elimu ya Afya (Health Communication)
- Mpango wa Huduma za Afya ngazi ya Jamii(Community Based Health Program)
- Program ya Afya Shuleni(National School health Program)
- Sehemu ya uchapaji (Printing unit)
- Sehemu ya Studio na uhifadhi (Studio and Resource centre)

Dira ya Seksheni ni:

- Kuwa na jamii yenye uwezo wa kuchambua na kufanya maamuzi yanayostahili kuhusu mtazamo, tabia na mwenendo wa maisha unaojenga na kuendeleza afya bora.

Mwelekeo wa Seksheni ni:

- Kujenga mazingira yanayowezesha elimu ya afya kutolewa kwa ubora ili kuelimisha na kuhimiza tabia na desturi zinazojenga na kuendeleza afya bora.

Wigo wa kazi na majukumu ya Seksheni ya Elimu ya Afya yamekua kulingana na wakati na mazingira ya sasa. Baadhi ya majukumu kwa sasa ni:

1. Kutengeneza na kupitia Miongozo ya Huduma za Elimu ya Afya mara kwa mara kulingana na mahitaji ya jamii.
2. Kupitia, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa Mwongozo na Sera ya utoaji wa Elimu ya Afya kwa jamii.
3. Kupitia na kuhakiki vielelezo ili kuboresha ubora wa ujumbe wa vielelezo vinavyo tengenezwa na wadau mbali mbali kwa ajili ya kuelimisha wananchi kuhusu masuala ya afya.

4. Kusaidia upangaji na utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Elimu ya Afya zinazolenga makundi mbali mbali katika jamii.
5. Kutoa ushauri wa kitaalamu kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa, Kanda na Wadau wengine ili kuboresha Huduma za Elimu ya Afya
6. Kupanga mikakati mbali mbali ya jinsi ya kukabiliana na majanga.
7. Kuandaa, na kuratibu shughuli za utafiti zinazolenga kuboresha utoaji wa Elimu ya Afya.
8. Kuratibu maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Afya Duniani na Siku ya kutotumia Tumbaku Duniani.
9. Kuandaa na kusambaza vielelezo mbali mbali vyenye ujumbe unaolenga kuboresha afya ya wananchi kupitia nji mbalimbali hasa kupitia mitandao ya kijamii (You tube, Facebook, Twitter na Instagram
10. Kuandaa vipindi vya redio kwa ajili ya kuelimisha jamii masuala ya Afya.

Mafanikio ya Kitengo ambayo kimeyapata ni pamoja na:

1. Tumeweza kuunda dawati la wanahabari la Elimu ya Afya toka katika vyombo mbalimbali vya habari, ambao tunashirikiana nao kwa karibu katika kuelimisha jamii masuala mbalimbali yanayohusu Afya.
2. Tumejenga ushirikiano na sekta binafsi, taasisi na asasi mbalimbali zinazojihusisha na shughuli mbalimbali za mawasiliano ya afya na utoaji wa Elimu ya Afya kwa Ujumla kama Wizara ya Elimu, Kilimo, Maendeleo ya Jamii na vyombo vya habari.
3. Kujenga uwezo wa watumishi katika kada zote, (kuwasomesha) katika ngazi mbalimbali.
4. Kuwa kamati ya uhakiki wa bora wa vielelezo na kuainisha majukumu yake
5. Mwaka 2013 hadi 2018 kitengo kilijengewa studio ya radio na televisheni chini yaufadhili wa WB ambacho kinafanya kazi hadi ssa katika ofisi zake Dar es Salaam.

6. Kitengo Kimekuwa kikipokea ufadhili wa vitendea kazi toka UNICEF, UNFPA, AMREF……katika kutekeleza majukumu yake
7. Kitengo kupitia ufadhili wa…….kimefungua kituo cha ‘Call Centre’ kinachofanya kazi saa 24, chenye watalaamu wa kutosha katika fani mbalimbali za afya, mwananchi anapiga namba **199**.

Changamoto zinazoikabili Seksheni ya Elimu ya Afya kwa Umma ni pamoja na:

- Kufikisha ujumbe sahihi kwa walengwa katika nyakati muafaka.
- kuzingatia viwango na ubora wa vielelezo vya elimu ya afya, katika kukabilina na hilo tumeunda Kamati ya Kitaifa ya Uhakiki wa Vielelezo vya mawasiliano ya afya.
- Kuboresha vitendea kazi mfano mashine za uchapishaji, kuwa na studio yenye vifaa vya kisasa pamoja na magari maalum (mobile van) ya kufanyia kampeni mbalimbali za kuelimisha jamii hasa nyakati za milipuko ya maradhi.
- Kuzidi kuboresha uratibu na ushirikiano miongoni mwa wadau mbalimbali wa mawasiliano ya afya
- Uhaba wa watumishi kukidhi mahitaji yake
- Uhaba wa vitendea kazi